# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA WAZIRI WA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

**MHESHIMIWA MASOUD ALI MOHAMMED (MBM)**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**ILIYOWASILISHWA MBELE YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI, 2026**

## YALIYOMO

A. UTANGULIZI ..........................................................1

B. MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA.................................................. 5

C. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI..................................................6

D. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/202 .............................................16

E. CHANGAMOTO ..................................................41

F. MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.........................................................42

G. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA PROGRAMU KUU P01: MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU ......................................................46

H. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA PROGRAMU KUU P02: MAENDELEO YA UVUVI............................................................51

I. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA PROGRAMU KUU P03: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI............................................................61

J. MAOMBI YA KUIDHINISHIWA MAPATO NA MATUMIZI KWA FUNGU LA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI (013) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ..........................65

K. SHUKRANI.................................................................67
L. HITIMISHO...............................................................69
VIAMBATANISHO ..................................................70

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai, uzima na kutukutanisha hapa tukiwa na afya njema tukaweza kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu hii leo kuwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvvi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zao wanazozichukua kudumisha amani, utulivu, mshikamano na kuleta maendeleo ya Taifa letu.

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda nichukue nafasi hii kuendelea kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuchaguliwa kwa

ushindi mkubwa kwa nafasi za urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na urais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, hii inatokana na imani kubwa ya wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kutokana na uongozi wao shupavu na maono yao ambayo yamepelekea kuwa na uongozi uliotukuka.

5. **Mheshimiwa Spika,** Kipekee nitumie fursa hii kwa heshima na unyeyekevu mkubwa, kumshukuru sana Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini kwa kuniteua kuwa Mjumbe wa Baraza hili na kuniteua kushika dhamana ya Uwaziri wa Wizara hii. Ninamuahidi kuitumikia dhamana hii kwa uadilifu na uwajibikaji kwa maslahi mapana ya wananchi wenzetu na Taifa kwa ujumla.

6. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa mashirikiano yake anayotupatia katika kuendeleza majukumu ya Wizara hii. Aidha, nimpongeze kwa dhati kwa kuchaguliwa kwake na wananchi wa jimbo la Kiwani kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na kuendelea kuaminiwa kwa kiwango kikubwa na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa kwa kipindi cha pili kuwa mtendaji mkuu wa shughuli za Serikali.

7. **Mheshimiwa Spika,** Shukrani maalum ziende kwa Waziri alienitangulia kwenye Wizara hii ambae ni Mheshimiwa Shaaban Ali Othman, Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji kwa uongozi wake uliojenga misingi imara katika kuendeleza Wizara hii. Wizara inathamini jitihada zake za kujenga mshikamano, kuimarisha utendaji na kusimamia vyema majukumu ya Wizara.

8. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa umahiri, uweledi na ujasiri wa kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa hekima, busara na maono makubwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na anavyoendelea kusaidia kuliongoza Baraza hili kwa umakini. Kadhalika, nawapongeza Wenyeviti wa Baraza Mheshimiwa Dkt. Mahmoud Omar Hamad Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Tumbatu na Mheshimiwa Hudhaima Mbarak Tahir Mwakilishi wa Viti Maalum kwa umahiri wao mkubwa wa kuendesha vikao vya Baraza la Wawakilishi. Vilevile, namshukuru na kumpongeza Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndugu Raya Issa Mselem kwa mashirikiano makubwa anayotupatia.

9. **Mheshimiwa Spika,** natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Makame Mohamed Sufiani Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Chumbuni kwa kuchaguliwa

kuiongoza Kamati ya Uchumi na Uwekezaji. Uongozi wake, hekima, busara na uadilifu umeisaidia Wizara katika kutekeleza majukumu yake.

10. **Mheshimiwa Spika,** shukurani na pongezi pia ziwaendee Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Uwekezaji Dkt. Mahmoud Omar Hamad Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Tumbatu na Wajumbe wa Kamati wakiwemo; Mheshimiwa Shafi Mohammed Shafi mwakilishi wa wananchi jimbo la Wete, Mheshimiwa Chumu Kombo Khamis mwakilishi wa viti maalum Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mheshimiwa Alley Masoud Alley mwakilishi wa wananchi jimbo la Mtambile, Mheshimiwa Tabia Maulid Mwita mwakilishi wa viti maalum Mkoa wa Mjini Kichama, Mheshimiwa Taufiq Salim Turky mwakilishi wa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na makatibu wa Kamati akiwemo Ndugu Talib Enzi Talib, Ndugu Abdu Maulid Haji, na Ndugu Shaabani Suleiman Juma kwa mashirikiano makubwa wanayotupatia.

11. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kutumia fursa hii kukishukuru na kukipongeza Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa misingi ya amani, umoja na maendeleo. Aidha, ninakishukuru Chama hiki kwa kuendelea kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2025–2030 ambayo imeendelea kuwa

dira muhimu ya maendeleo ya Taifa letu na ustawi wa wananchi.

12. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo ulioambatana na shukurani na pongezi, naomba uniruhusu sasa kuwasilisha hotuba yangu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

## B. MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### Mapato ya Wizara

13. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilikadiriwa kukusanya **Shilingi 11,273,214,000** kutoka vyanzo vyake vya makusanyo na hadi kufikia Machi 2026, Wizara imefanikiwa kukusanya **Shilingi 8,493,203,472** kati ya **Shilingi 9,261,573,363** zilizokadiriwa sawa na **asilimia 92** kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi, 2025/2026). Makusanyo hayo ni sawa na **asilimia 75** ya makadirio ya mwaka **(Kiambatanisho nambari 1).**

### Upatikanaji wa Fedha za Matumizi

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ililiomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha **Shilingi 172,033,961,377** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

Kati ya fedha hizo, **Shilingi 14,952,100,000** ni kwa kazi za kawaida na **Shilingi 157,081,861,377** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, Wizara imeingiziwa jumla ya **Shilingi 35,116,155,652** sawa na **asilimia 20.4** ya makadirio ya mwaka ambayo ni sawa na **asilimia 24.3** kwa kipindi cha miezi tisa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 10,182,888,829** ni kazi za kawaida ambapo **Shilingi 2,941,322,784** ni mishahara, **Shilingi 4,725,666,471** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo **(Shilingi 3,746,197,541** ni fedha zinazotokana na gawio la makusanyo ya maeneo ya hifadhi na **shilingi 979,468,930** ni matumizi ya OC), **Shilingi 2,515,899,574** ni ruzuku ya mshahara na matumizi ya kawaida kwa Taasisi zinazojitegemea na **Shilingi 24,933,266,823** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo **(Kiambatanisho nambari 2).**

## C. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI.

15. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imetekeleza malengo yake kupitia Programu Kuu tatu (3) na Programu ndogo saba (7) ambazo ni:

i. Programu Kuu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu;

- Programu ndogo ya Uratibu na Maendeleo ya Uchumi wa Buluu

- Programu ndogo ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia.

ii. Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi;

- Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini.
- Program ndogo ya uhifadhi wa Rasilimali za bahari

iii. Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

- Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji.
- Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti.
- Program ndogo ya kazi za uchumi wa Buluu Pemba.

16. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hizi, Wizara imefanikiwa kutekeleza malengo yake na kupata mafanikio katika mambo yafuatayo:

1) **Ujenzi wa Miundombinu ya Bandari za Uvuvi, Madiko, Viwanda, Huduma na Biashara za Uchumi wa Mazao ya Baharini.**

17. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza ujenzi wa miundombinu ya bandari, Wizara imekamilisha zoezi la Upembuzi Yakinifu (Feasiblity Study) na michoro ya bandari, na sasa Wizara ipo katika hatua ya kufanya Tathmini ya Kiuchumi ya uwekezaji wa bandari ya

uvuvi kwa eneo husika. Aidha, Wizara imefanya mazungumzo na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Shirika la Bandari kwa ajili ya kuanza hatua za kuifanya bandari inayojengwa Shumba Mjini kuwa bandari jumuishi ya Mizigo na Shuguli za Uvuvi.

18. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha miundombinu ya madiko ya kisasa ya Samaki, Wizara imeendelea kutekeleza kwa mafanikio makubwa uwekaji wa miundombinu ya madiko ya kisasa ya Samaki kwa kukamilisha ujenzi wa diko la kisasa la samaki Mkoani Pemba lenye uwezo wa kuhudimia watumiaji zaidi ya 10,000 pamoja na boti za uvuvi 250 kwa siku, kuhifadhi tani 30 za samaki katika viwango tofauti vya baridi na kuzalisha tani 5 za barafu kwa siku, hatua inayochangia kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi na kuongeza thamani ya bidhaa. Diko hilo pia lina miundombinu saidizi ikiwemo maduka na ofisi, hivyo kuchochea shughuli za biashara naajira kwa wananchi. Pia, Wizara inaendelea na ujenzi wa diko la kisasa la samaki Fungurefu ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 80. Aidha, ujenzi wa madiko mengine matano (5) umeanza katika maeneo ya Kiwani, Msuka na Kengeja kwa Pemba na Pitanazako na Fukuchani kwa Unguja, ikiwa ni jitihada za kuimarisha zaidi mnyororo wa thamani wa sekta ya uvuvi nchini.

19. **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kukuza uchumi wa viwanda na kuongeza thamani ya rasilimali za

baharini, Wizara kupitia Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) inaendelea na ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa katika eneo la Ndagoni Pemba kwa awamu ya kwanza, ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 60. Aidha, Wizara imeanzisha eneo maalumu la uwekezaji wa Uchumi wa Buluu katika eneo la Fungurefu lenye ukubwa wa hekta 235, ambapo hatua ya sasa ni kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi ili kuweka mazingira wezeshi kwa uwekezaji na kuchochea maendeleo ya sekta za Uchumi wa Buluu.

20. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha huduma na biashara za uchumi wa mazao ya baharini, Wizara imefanikiwa kuongeza uzalishaji wa samaki kutoka tani **78,943** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 618.18** mwaka 2024 hadi kufikia tani 79,431 zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 624.9** mwaka 2025, sawa na ongezeko la **asilimia1.4.** Ongezeko hili limechochea upatikanaji wa malighafi kwa shughuli za biashara, kuimarisha masoko ya mazao ya baharini na kuongeza kipato kwa wavuvi na wadau wengine katika mnyororo wa thamani. Wizara imefanikiwa kuongeza uzalishaji wa mwani mkavu kutoka tani **19,716** mwaka 2024 hadi kufikia tani **20,075** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 14.253** mwaka 2025. Sambamba na hilo, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, jumla ya tani **8,055** za mazao ya baharini yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 27.333** zimesafirishwa nje ya nchi.

**21. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kurahisisha na kuharakisha utoaji wa vibali pamoja na kupunguza vikwazo vya usafirishaji wa mazao ya baharini, Wizara imeanza kuandaa mfumo wa kidijitali utakaounganisha utoaji wa leseni na usimamizi wa vibali vya kusafirishia mazao hayo na taasisi husika ikiwemo Shirika la Bandari Zanzibar na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar. Hatua hii itasaidia kuleta ufanisi zaidi, kupunguza muda na gharama za biashara, kuongeza uwazi na uwajibikaji, na hatimaye kuimarisha ushindani wa bidhaa zetu katika masoko ya Kikanda na Kimataifa.

### 2) Uwezeshaji na Uwekezaji katika Uvuvi Endelevu wa Mwambao na Bahari Kuu, Kilimo cha Mwani na Ufugaji wa Viumbe Maji

**22. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza uwekezaji katika uvuvi endelevu wa mwambao na bahari kuu, Wizara imefanikiwa kukamilisha sehemu kubwa ya mchakato wa manunuzi wa meli kubwa za kisasa za uvuvi wa bahari kuu kwa lengo la kuendeleza jitihada za uvuvi wa Bahari kuu na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa samaki ili kukuza pato la Taifa.

**23. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha na kulipa hadhi zaidi zao la mwani, Wizara imekamilisha hatua za ukamilishaji na utumikaji Kiwanda cha Mwani Chamanangwe, ikiwemo ununuzi wa Mashine pamoja na kuanza hatua za kukamilisha kazi za nje (external works) za kiwanda hicho. Sambamba na hilo, hatua

za uanzishwaji wa Kiwanda cha mwani cha kuzalisha virutubisho vya chakula (food supplement) na bidhaa nyenginezo zimeanza, ambapo hatua za kuangiza mitambo ya kiwanda hicho zimeshaanza na kiwanda hicho kitaendeshwa kwa ubia baina ya Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO) na Kampuni binafsi. Aidha, Wizara imenunua mashine tano zenye uwezo wa kuchakata tani 5 za mwani kwa siku ambazo tayari zimewasili, na hatua inayoendelea ni ujenzi wa miundombinu ya kuzifunga ili kuanza uzalishaji.

24. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha soko na ubora wa zao hilo, Wizara imejenga makaushio (solar driers) ya kisasa katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba, ikiwemo Jongowe na Makangale, Muungoni na Kiuyu, pamoja na kuwapatia wakulima wa mwani 10,085 vifaa na mafunzo ya kilimo bora cha kisasa kwa lengo la kuongeza tija na ubora wa zao hilo. Jitihada hizi zimechangia kuongezeka kwa uzalishaji wa mwani kutoka tani 19,716 mwaka 2024 hadi tani 20,075 mwaka 2025, sawa na ongezeko la **asilimia 1.8.**

25. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uwezeshaji wa shughuli za ufugaji wa viumbe maji, Wizara imegawa jumla ya vifaranga 60,000 vya majongoo bahari kwa vikundi 17 kutoka Unguja na Pemba. Hatua hii inalenga kuongeza uzalishaji, kukuza kipato cha wanavikundi na kuimarisha mchango wa ufugaji wa viumbe maji katika uchumi wa buluu.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuimarisha usimamizi bora na endelevu wa matumizi ya rasilimali za uvuvi, Wizara imewasilisha Serikalini Waraka wa Mapendekezo ya kufuta Sheria ya Uvuvi nambari 7 ya mwaka 2010 na kutunga Sheria ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari Zanzibar. Kukamilika kwa Sheria hii kutapelekea kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari Zanzibar. Hatua iliyopo sasa ni kuwasilishwa Mswada wa Sheria hiyo katika Baraza la Wawakilishi.

### 3) Utafiti wa Uvuvi, Sayansi za Bahari, Maliasili za Bahari, Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi Baharini.

**27.** **Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuimarisha utafiti wa uvuvi, sayansi za bahari na usimamizi wa maliasili za baharini, Wizara imefanikiwa kuanzisha maabara ya kisasa ya uzalishaji wa mbegu bora za Mwani kwa njia ya upandishaji wa mbegu (Tissue Culture Laboratory) ambayo itawezesha upatikanaji wa mbegu bora zenye uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi na mazingira magumu. Sambamba na juhudi hizo za utafiti, Wizara imeanzisha vitalu vya mwani ili kuwezesha upatikanaji wa mbegu kwa wakulima wa mwani Unguja na Pemba ambapo jumla ya kilogramu 4,929 za mbegu za mwani zimevunwa na kugaiwa kwa wakulima wa mwani.

### 4) Usimamizi wa Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari

28. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuimarisha usimamizi wa hifadhi za bahari, Wizara imefanikiwa kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Hifadhi mbili (2) Mashariki mwa kisiwa cha Pemba (Kusini Mashariki na Kaskazini Mashariki) zenye ukubwa wa kilomita 1,300, hatua inayolenga kulinda rasilimali za baharini. Aidha, Wizara imendelea kuimarisha ulinzi wa maeneo ya hifadhi kwa kuanzisha kituo kipya cha doria katika Kisiwa cha Bawe na kuanza kazi kwa vituo vitatu (3) vya doria vilivyopo Michamvi, Pungume na Msuka. Sambamba na hayo, Wizara imenunua boti za kisasa tisa (9) kwa ajili ya doria na utafiti wa baharini ambapo boti saba (7) ni maalum kwa ajili ya doria na boti mbili (2) zitatumika kwa shughuli za Utafiti wa baharini. Vilevile, ushirikishwaji wa jamii umeimarishwa kupitia mafunzo kwa Kamati za Usimamizi Shirikishi kwa lengo la kuimarisha ulinzi na uhifadhi endelevu wa mazingira ya bahari.

29. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na jitihada za kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa hifadhi za bahari, Wizara imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na hifadhi za bahari ambapo jumla ya **Shilingi 7,220,886,958** zimekusanywa kwa kipindi cha miezi tisa (9) (Julai – Machi 2026) kati ya Shilingi 7,008,038,025 zilizokadiriwa kwa mwaka, sawa na asilimia 103 kwa mwaka. Mafanikio haya yanaonesha ufanisi mkubwa

wa usimamizi wa hifadhi zetu na yanadhihirisha kuimarika kwa hifadhi hizi kama kivutio kikubwa cha utalii, ambapo takwimu zinaonesha kuwa takribani nusu ya watalii waliokuja Zanzibar mwaka jana walitembelea hifadhi hizo, hali inayoonesha umuhimu wa kuendelea kuzilinda na kuzisimamia kwa ufanisi ili kuongeza tija ya kiuchumi na kuendelea kuwa kivutio kwa wageni wanaotembelea nchi yetu na kubakia kuwa urithi muhimu kwa vizazi vijavyo.

**5) Kuendeleza jitihada za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia.**

30. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza shughuli za Utafutaji na Uchimabaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Wizara imefanikiwa kuingia mikataba ya tafiti za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia ikiwemo utafiti wa mtetemo wa 3D kwa nchi kavu (kitalu cha Z2 – Unguja) kupitia Kampuni ya Africa Geophysical Services (AGS) kutoka Oman, utafiti wa mtetemo wa 2D kwa baharini kupitia Kampuni ya SLB kutoka Uingereza, na utafiti wa maeneo yanayovuja mafuta baharini kupitia Kampuni ya Geopartners kutoka Uingereza. Hatua hizi, zinalenga kupata taarifa muhimu na za uhakika kitaalamu kwa ajili ya kujua maeneo ya kuchimba visima na kuweka msingi mzuri wa kuvutia uwekezaji. Aidha, miundombinu ya usimamizi wa Taarifa (Data) za Mafuta na Gesi Asilia ikiwemo ujenzi wa kituo maalumu cha kuhifadhia na kukagulia taarifa imekamilika.

31. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wizara imeendelea kuvitangaza vitalu 10 vya Mafuta na Gesi Asilia (8 baharini na 2 nchi kavu) katika majukwaa mbali mbali ya Uwekezaji na kuendelea na majadiliano na wawekezaji wa kimataifa kwa ajili ya kuingia Mikataba ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia. Aidha, fidia kwa wananchi walioathirika na tafiti za awali imelipwa.

6) **Utoaji wa elimu na uelewa katika masuala ya Uchumi wa Buluu ikiwemo mbinu, nyenzo, mitaji na utafutaji wa masoko kwa wajasiriamali na wananchi kwa ujumla.**

32. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uelewa wa wadau kuhusu fursa za Uchumi wa Buluu, ikiwemo mbinu bora, upatikanaji wa nyenzo, mitaji na masoko, Wizara imefanikiwa kuwafikia wananchi mbali mbali kupitia programu mbali mbali ikiwemo mikutano, semina, warsha, na makongamano kwa Unguja na Pemba kwa lengo la uelimishaji, hatua inayochangia kukuza ushiriki na uendelezaji wa shughuli za uchumi wa buluu.

7) **Usimamizi wa Bahari (Usalama wa Bahari, Kuimarisha Ulinzi wa Bahari na Kupambana na Uvuvi Haramu Usioripotiwa).**

33. **Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuhakikisha usimamizi endelevu wa bahari, Wizara imekamilisha

Mkakati wa Mawasiliano (Communication Strategy) wa utekelezaji wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Bahari (Marine Spatial Planning – MSP) wenye lengo la kuweka mfumo wa mawasiliano ya wadau katika utekelezaji wa Mpango wa Matumizi bora ya Bahari pamoja na uchambuzi wa taarifa (data) zinazohitajika katika utekelezaji wa Mpango huo.

34. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ulinzi na usalama wa bahari, Wizara kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya Ulinzi na Usalama imefanya doria 249 za kudhibiti uvuvi haramu kwa Unguja na Pemba kwa lengo la kuimarisha Ulinzi wa Bahari na kupambana na Uvuvi Haramu na Usioripotiwa. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA), imefanikiwa kuimarisha ulinzi na usalama wa bahari kuu kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ya ufuatiliaji wa mienendo ya meli (Vessel Monitoring System - VMS na Automatic Identification System – AIS) ambao huwezesha kutambua shughuli zinazofanywa na vyombo vya uvuvi kitaalamu.

## D. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

35. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imetekeleza majukumu yake kupitia Mfumo wa Bajeti unaotumia Programu (PBB) kupitia fungu moja la bajeti (L02) lenye Programu Kuu tatu (3) ambazo ni

Programu Kuu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu (PL0201), Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi (PL0202) na Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara (PL0203).

## PROGRAMU KUU PL0201: MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

36. **Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Programu kuu hii ni kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu pamoja na kusimamia shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia. Programu hii imegawika katika Programu ndogo mbili ambazo ni Programu Ndogo ya Uratibu na Maendeleo ya Uchumi wa Buluu (SL020101) na Programu Ndogo ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia (SL020102).

37. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu hii ilipangiwa jumla ya **Shilingi 26,740,300,000.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 4,165,300,000** ni kwa matumizi ya kawaida na **Shilingi 22,575,000,000** kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, programu hii imepatiwa jumla ya **Shilingi 15,866,074,529** sawa na **asilimia 59.3** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,724,829,329** ni kwa matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 41.4 ya** makadirio na **Shilingi 14,141,245,200** kwa miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 62.6 (Kiambatanisho nambari 2).**

### i. Programu Ndogo ya Uratibu na Maendeleo ya Uchumi wa Buluu (SL020101).

38. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai – Machi cha mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Uratibu na Maendeleo ya Uchumi wa Buluu imetekeleza yafuatayo:

a) Imekamilisha Mpango wa Matumizi ya Zoni 3 na 5 zilizopo katika Hifadhi ya Bahari ya Magharibi mwa Kisiwa cha Pemba (Pemba Channel Conservation Area – PECCA).

b) Imekamilisha Mkakati wa Mawasiliano (Communication Strategy) wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Bahari (Marine Spatial Planning - MSP).

39. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu Ndogo hii imeombewa jumla ya **Shilingi 7,201,500,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 200,000,000** kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 426,500,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 6,575,000,000** kwa utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo kutoka SMZ. Hadi kufikia Machi 2026, programu hii imepatiwa jumla ya **Shilingi 184,282,813**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 70,727,375** ni mshahara na **Shilingi 113,555,438** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi sawa na **asilimia 26.6** ya makadirio ya mwaka.

**ii. Programu ndogo ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia (SL020102).**

40. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai – Machi cha mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia ilitekeleza yafuatayo: -

a) Imekamilisha kazi ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2016 kwa lengo la kubaini ufanisi wake wa kuendana na vipaumbele vya mipango ya maendeleo ya Zanzibar, mabadiliko ya kitaifa na kimataifa katika sekta ya mafuta na gesi asilia.

b) Imetangaza fursa za uwekezaji wa vitalu vya mafuta na gesi asilia vya Zanzibar kupitia jarida (magazine) la ZiBi linalosambazwa katika zaidi ya nchi 10 za Asia, Afrika, Ulaya na Marekani. Miongoni mwa Nchi hizo ni Oman, Kuwait, Qatar, Bahrain, Marekani, Canada, Uingereza, Ujerumani, Uholanzi na Afrika Kusini.

c) Imeratibu na kuendesha majadiliano (negotiations) na Kampuni mbili (2) za Kimataifa za mafuta na gesi asilia kwa lengo la kuingia Mikataba ya shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia Zanzibar. Aidha, Wizara imefanikiwa kuingia mkataba mmoja wa huduma za utafiti wa mtetemo kwa njia ya 3D na Kampuni ya Africa Geophysical Services (AGS) kutoka Oman na

maandalizi ya utekelezaji wake yanaendelea. Sambamba na hayo, majadiliano yanaendelea na kampuni nyingine mbalimbali zenye nia ya kuwekeza katika sekta ya mafuta na gesi asilia Zanzibar.

d) Imeendesha programu 6 kati ya 10 zilizopangwa za kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia kupitia vipindi vya televisheni pamoja na ushiriki katika maonesho ya Saba Saba Dar-es-Salaam, Nane Nane na Maonesho ya Biashara ya Nyamanzi.

**41.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu Ndogo ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia iliidhinishiwa kutumia **Shilingi 19,538,800,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,538,800,000** ni kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 90,000,000** ni Mishahara, **Shilingi 398,000,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 3,050,800,000** ni ruzuku kwa ajili ya Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA). Aidha, **Shilingi 16,000,000,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutelekeza Miradi ya Maendeleo kwa Programu hii.

**42.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2026 programu hii imeptaiwa jumla ya **Shilingi 15,681,791,716** sawa na **asilimia 80.3.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 40,955,655** ni matumizi ya uendeshaji wa Ofisi, **Shilingi 1,499,550,861** ni ruzuku kwa ajili ya

Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA) na **Shilingi 14,141,245,200** kwa ajili ya kutelekeza Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 88.4** ya makadirio kwa mwaka.

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPRA).**

**43.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) ina jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli zote za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Mamlaka ya ZPRA imetekeleza shughuli zifuatazo: -

a) Imeingia mkataba na Kampuni ya Geopartners kutoka Uingereza kwa ajili ya kuchukua taarifa za maeneo yanayovuja mafuta na gesi asilia katika maeneo ya baharini, na Kampuni ya SLB kutoka Uingereza kwa lengo kuchukua taarifa za mtetemo kwa njia ya 2D, mikataba ambayo itagharamiwa na Kampuni husika.

b) Imeingia Hati ya Makubaliano (MoU) baina ya Taasisi za Mamlaka ya Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) ya Tanzania Bara na Mamlaka ya Mafuta na Gesi Asilia ya Nchini Uganda (PAU) kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika usimamizi wa shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

c) Imekamilisha ulipaji wa fidia kwa Wananchi walioathirika na zoezi la Mtetemo wa njia ya 2D lililofanywa na Kampuni ya RAKGAS kwa Unguja na Pemba.

d) Imeshiriki katika mikutano miwili (2) ya Kimataifa ya utetezi wa maombi ya Tanzania kuhusu kuongeza eneo la nje ya ukanda maalumu wa kiuchumi (Extended Continental Shelf), Jijini New York, Marekani.

e) Imetekeleza shughuli za Ufuatiliaji na ukaguzi katika programu za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia ambapo jumla ya ziara 13 na mikutano saba (7) imefanyika Unguja, Pemba, Dar Es Salaam na Mtwara katika maeneo ya uzalishaji wa Gesi Asilia. Aidha, Wataalamu wawili (2) wa Mamlaka walishiriki zoezi la uchukuaji wa Taarifa za kijiolojia kwa njia ya mtetemo wa 2D katika maeneo ya utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia Mkoa wa Simiyu Tanzania Bara.

f) Imeendesha mafunzo kwa watendaji 18 yanayohusu Usimamizi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (Data) ikiwemo matumizi ya mifumo (software) kwa ajili ya kutafsiri data na kuchorea ramani (Arc Pro GIS na DB Map).

g) Imefanya programu 13 za kujenga uelewa kwa jamii kuhusu shughuli za Mafuta na Gesi Asilia kupitia magazeti (5), Televisheni na Redio (3),

Tasisi za Umma (3) na Maonesho mawili (2) ya kitaifa ya sherehe za miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja Maonesho ya Kilimo ya Nanenane.

44. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) iliidhinishiwa **Shilingi 10,050,800,000.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 1,942,100,000** kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 1,108,700,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 7,000,000,000** kwa utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2026, ZPRA imepatiwa jumla ya **Shilingi 1,499,550,861** sawa na **asilimia 14.9.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,135,809,041** ni mishahara na **Shilingi 363,741,820** kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi.

**KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPDC).**

45. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar ina jukumu la kushiriki katika biashara ya utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia kwa niaba ya Serikali. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia imetekeleza shughuli zifuatazo:

a) Imeingia Mkataba na Kampuni ya AGS (Africa Geophysical Company) kwa ajili ya kazi ya uchukuaji wa taarifa za mtetemo wa kina (3D

Seismic Data Acquisition) katika maeneo ya Paje na Kinyasini. Upatikanaji wa taarifa hizo utasaidia katika uchaguzi sahihi wa eneo la kuchimba visima vya majaribio vya mafuta na gesi asilia.

b) Imeanza hatua za awali za utoaji wa uelewa kwa wadau kuhusiana na Mradi wa Uchukuaji wa Taarifa kwa njia ya 3D kwa Mikoa ya Kaskazini na Kusini, zikihusisha Kamati za Ulinzi na Usalama, wananchi na wamiliki wa mashamba 1,110 watakaopitiwa na mradi huo, skuli 9 katika maeneo husika na Taasisi 16 za Serikali zikiwemo ZRA, ZIPA, ZANROAD, Wizara ya Ardhi, Kilimo na Wizara ya Kazi. Aidha, Tathmini za Athari za Kimazingira na Kijamii (ESIA) pamoja na Tathmini ya fidia kwa waathirika wa mradi tayari zimeshaanza.

c) Imeimarisha mazingira bora ya kiutendaji ya Kampuni kwa kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mfupi kuhusiana na Mafuta na gesi asilia, ununuzi wa vifaa na mifumo ikiwemo software kwa uchambuzi na uendeshaji wa shughuli za mafuta na gesi Asilia.

**46.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia iliidhinishiwa **Shilingi 9,000,000,000** kutoka SMZ kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, Kampuni imepatiwa jumla ya

**Shilingi 14,141,245,200** sawa na **asilimia 157** kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maendeleo.

## PROGRAMU KUU PL0202: MAENDELEO YA UVUVI

**47.** **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi ina lengo la kuimarisha maendeleo ya sekta ya uvuvi na uhifadhi wa bahari ili kuboresha maendeleo endelevu ya jamii. Programu hii imegawika katika Programu Ndogo mbili (2) ambazo ni Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini (SL020201) na Programu ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Baharini (SL020202).

**48.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 141,628,761,377.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 7,121,900,000** kwa Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 134,506,861,377** kwa Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 108,670,370,000** kutoka SMZ na **Shilingi 25,836,491,377** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, Programu hii imepatiwa **Shilingi 16,959,170,521.** Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 1,191,552,587** ni mishahara, **Shilingi 3,959,247,598** ni kwa kazi za kawaida sawa na **asilimia 105.5** ya makadirio, **Shilingi 1,016,348,713** ni ruzuku kwa Taasisi ya ZAFIRI sawa na **asilimia 64.7** ya makadirio na **Shilingi 10,792,021,623** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo **(Kiambatanisho nambari 2).**

i. **Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini (SL020201).**

49. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu Ndogo hii imetekeleza shughuli zifuatazo:

a) Imekamilisha ujenzi wa Diko la kisasa la Samaki, Mkoani Pemba. Aidha, ujenzi wa Diko la kisasa la Fungurefu, Mkokotoni unaendelea ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2026 umefikia wastani wa asilimia 80 ya utekelezaji.

b) Imejenga mashamba darasa mawili (vitalu 2) ya kilimo cha mwani [Muungoni na Pwani Mchangani] yanayotumika kwa ajili ya kutoa huduma za utafiti wa kitaaluma kuhusu sababu zinazochangia mwani kushambuliwa na maradhi na kushindwa kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

c) Imefanya usajili wa wavuvi kwa kutoa leseni za kisasa za kielektroniki ambapo hadi sasa wavuvi 964 wamesha sajiliwa kwa lengo la kuwatambua na kuimarisha huduma za shughuli za uvuvi.

d) Imewapatia huduma za Ugani kwa Wakulima wa Mwani 100 kutoka Wilaya ya Kusini na Magharibi B na wafugaji wa mazao ya baharini 100 kwa Wilaya zote za Unguja kwa lengo la kuimarisha uzalishaji wa mazao yao.

e) Imewawezesha wakulima wa mwani 6,288 kwa kuwapatia boti ndogo (vihori) 150 kwa ajili ya

kubebea mwani. Aidha, jumla ya vifaranga 60,000 vya majongoo bahari vimegaiwa kwa vikundi 17 kutoka Unguja na Pemba. Vikundi hivyo ni Ulezi kazi, Nia Njema, Uvivu si Mtaji, Stahamili, Innur, Tumuombe Mola, Tuelewane, Jiongeze Group, Mtu ni Yupi, Mojongoo Wambaa, Jitihada, Mtu kwao, Ukunjwi Marine Conservation, Yataka moyo na Almujitahidi.

50. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 137,928,761,377.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,421,900,000** kwa Matumizi ya Kawaida (ambapo **Shilingi 1,100,000,000** ni Mishahara, **Shilingi 752,000,000** ni Matumizi ya Uendeshaji ya Ofisi na **Shilingi 1,569,900,000** ni ruzuku kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI) na Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO)), na **Shilingi 134,506,861,377** kwa kutekeleza miradi ya maendeleo (ambapo **Shilingi 108,670,370,000** kutoka SMZ na **Shilingi 25,836,491,377** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, Programu hii imepatiwa **Shilingi 11,959,250,632**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,162,185,975** ni mishahara, **Shilingi 133,413,946** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 10,663,650,711** ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za maendeleo **(Kiambatanisho nambari 2)**.

## TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MALIASILI ZA BAHARINI ZANZIBAR (ZAFIRI)

51. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar imetekeleza shughuli zifuatazo: -

a) Imetekeleza mradi wa Asia-Africa BlueTech Super-Highway (AABS), ambao kupitia Mradi huo Vyombo vya Wavuvi wadogo wadogo 100 [Unguja 60 na Pemba 40] wamefungiwa vifaa vya Pelagic Data System (PDS) na kupatiwa mafunzo ya matumizi ya vifaa hivyo ambavyo vinawezesha kujua maeneo ya Uvuvi (Fishing Grounds) kwa lengo la kuimarisha usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari.

b) Imeanzisha vitalu vya mbegu za mwani na kuwezesha upatikanaji wa mbegu za mwani kwa wakulima katika maeneo ya Kaskazini Unguja, ambapo jumla ya kilogramu 4,929 sawa na tani 4.9 za mbegu za mwani zimevunwa na kupatiwa wananchi kwa vikundi 24 sawa na wakulima wa mwani 395. Miongoni mwa vikundi hivyo ni pamoja na Tuwe na Umoja, Baya letu Cooperative, Sasa ni Kweli, Tunajiamini, Hidayatu Minallah, Ndugu Tupendane, Sema nao na Tunamuomba Mungu.

c) Imefanya utafiti wa kuangalia ikolojia katika kisiwa cha Changuu ili kujua hali halisi ya rasilimali za baharini zilizopo katika kisiwa hicho.

d) Imeratibu na kushiriki katika utafiti wa kuangalia hali halisi ya mazingira ya bahari kupitia Meli ya Utafiti ya Nansen katika Bahari ya Tanzania ikiwemo visiwa vya Unguja, Pemba na Mafia kwa lengo la kujua ikolojia za maliasili za baharini.

e) Imeimarisha Miundombinu ya Maabara za uthaminishaji wa bidhaa za baharini, pamoja na Maabara za uzalishaji wa mbegu za Mwani kwa kuongeza vifaa vya kisasa katika Maabara hizo.

f) Imefanya ufuatiliaji wa taarifa za tabia za Bahari katika maeneo ya bahari ya Zanzibar kupitia mifumo ya Sensors ziliwekwa katika Bandari za Malindi na Mkoani, pamoja na Boya liliwekwa katika maeneo Eneo la hifadhi ya Changuu-Bawe (Changuu-Bawe Marine Conservation Area – CHABAMCA).

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,153,500,00.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 794,900,000** ni Mishahara, **Shilingi 345,600,000** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 13,000,000** kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo ikiwa ni fedha za wahisani. Hadi kufikia Machi 2026, Taasisi ya ZAFIRI imepatiwa jumla ya **Shilingi 659,677,213** sawa na **asilimia 57.8.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 582,625,025** ni mishahara, **Shilingi 77,052,188** ni

matumizi mengineyo na **Shilingi 13,000,000** ni kwa ajili ya kumalizia sehemu ya mradi wa Utafiti wenye lengo la Kudumisha Uchumi, Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii.

**KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR (ZAFICO)**

53. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uvuvi Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, imetekeleza shughuli zifuatazo: -

    a) Inaendelea na usimamizi wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa kilichopo Ndagoni Pemba kwa awamu ya kwanza ambapo mradi huu umefikia **asilimia 60.**

    b) Imekamilisha hatua za awali za ujenzi wa kiwanda cha uzalishaji wa barafu na mitambo ya baridi pamoja na ujenzi wa jengo la wajasiriamali na mama lishe katika diko la Malindi.

54. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kampuni ya Uvuvi iliidhinishiwa **Shilingi 51,429,400,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 429,400,000** ni ruzuku ya Mishahara na **Shilingi 51,000,000,000** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, Kampuni imepatiwa jumla ya **Shilingi 485,042,412**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 356,671,500** ni ruzuku ya mishahara na **Shilingi 128,370,912** kwa ajili ya kazi za maendeleo.

## MAMLAKA YA KUSIMAMIA UVUVI WA BAHARI KUU (DSFA)

**55. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu imetekeleza shughuli zifuatazo:

a) Imetoa jumla ya leseni 42 za uvuvi wa bahari kuu (leseni 40 kwa meli za kigeni na leseni mbili (2) kwa meli za Kitanzania), vibali 24 vya kuvua nje ya mipaka ya Tanzania (Areas beyond national jurisdiction), vibali viwili (2) vya uwakala wa meli, na vibali saba (7) kwa meli saidizi (supporting vessel) na kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni 7.5.

b) Inaendelea kufanya utafiti wa kutambua wingi na mtawanyiko wa samaki aina ya Jodari katika maji ya Tanzania kwa kushirikiana na taasisi za utafiti nchini zikiwemo TAFIRI na ZAFIRI. Aidha, Mamlaka ya DSFA inaendelea kufuatilia mwenendo wa uvuvi katika Ukanda wa Kiuchumi wa Bahari kwa kukusanya takwimu za uvuvi.

c) Inafanya ufuatiliaji wa mienendo ya meli za uvuvi wa bahari kuu kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ya ufuatiliaji (Vessel Monitoring System - VMS na Automatic Identification System – AIS) kwa lengo la kusimamia shughuli zote za uvuvi wa bahari kuu. Sambamba na hilo, Mamlaka imeanza hatua za awali za mradi wa majaribio wa ufuatiliaji wa Kielekroniki (Electronic

Monitoring System - EMS) kwa kushirikiana na TNC na USAID - Heshimu Bahari.

### ii. Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari (SL020202)

56. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, imetekeleza shughuli zifuatazo: -

a) Imekamilisha taratibu za uanzishwaji wa hifadhi mbili (2) Pemba Mashariki (Kusini Mashariki na Kaskazini Mashariki) zenye ukubwa wa kilomita 1,300.

b) Imefanya Doria 174 za kudhibiti uvuvi haramu kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa shughuli za uvuvi na maeneo ya hifadhi. Aidha, boti saba (7) za kisasa za Doria zimenunuliwa kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu.

c) Imekamilisha ujenzi wa kituo cha doria Msuka kwa lengo la kuimarisha ulinzi na kuongeza uzalishaji wa mazao ya baharini. Aidha, vituo viwili (2) vya doria katika maeneo ya Michamvi na Pungume vimeanza kazi rasmi. Sambamba na hilo, kituo kipya cha doria katika Kisiwa cha Bawe kimeanzisha kwa madhumuni ya kuimarisha ulinzi wa maeneo ya hifadhi.

d) Imezijengea uwezo Kamati za usimamizi shirikishi (21) za jamii juu ya uhifadhi na

usimamizi wa mazingira na rasilimali za bahari ili kuimarisha mazingira na afya ya rasilimali za bahari kwa maslahi ya sekta ya uvuvi, ufugaji wa viumbe maji, ukulima wa mwani na utalii.

e) Imefanya ufuatiliaji wa matumbawe katika eneo la Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Tumbatu (Tumbatu Marine Conservation Area – TUMCA), Eneo la Hifadhi ya Ghuba ya MENAI (Menai Bay Conservation Area – MBCA) na eneo la Hifadhi ya bahari liliopo Magharibi mwa Kisiwa cha Pemba – PECCA (Misali, Matumbini na Kwata). Ufuatiliaji huo umebainisha kuwa matumbawe yameanza kujirudia baada ya kupauka kulikosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi.

f) Imeweka jumla ya Matumbawe bandia 1,907 katika maeneo ya Hifadhi za bahari katika Kisiwa cha Mnemba– MIMCA (Kisiwa cha Hifadhi ya Mnemba, Uroa na Pongwe), TUMCA (Donge Muwanda, Mto wa Pwani na Kiongwe), MBCA (Muyuni na Kizimkazi Mkunguni) na PECCA (Msuka na Kukuu) ili kurejesha afya ya bahari.

g) Imeandaa Kanuni inayotoa muongozo kwa Kamati za Uvuvi (SFC) na Kamati za Usimamizi za Pamoja (CMG) kutengeneza Sheria ndogo ndogo (bylaws) za Kamati hizo kwa ajili ya kusimamia maeneo madogo madogo wanayoyahifadhi.

h) Imeandaa muongozo wa waongozaji watalii na makepteni wa maboti ya utalii juu ya namna bora ya kufanya utalii wa pomboo na utalii wa kiti cha pweza katika hifadhi ya MIMCA. Aidha, mabango 25 yenye ujumbe wa kuhifadhi viumbe adimu na vilivyo hatarini kutoweka yaliwekwa katika maeneo yote ya Hifadhi ya Unguja na Pemba ili kuongeza uelewa kwa wavuvi na watumiaji wengine wa bahari.

**57.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, programu hii imeombewa **Shilingi 3,700,000,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 700,000,000** ni Mishahara na **Shilingi 300,000,000** ni Matumizi mengineyo (OC) na **Shilingi 2,700,000,000** “Retention” ya Makusanyo ya Idara ya Uhifadhi. Hadi kufikia Machi 2026, programu hii ilipatiwa jumla ya **Shilingi 3,855,200,264** sawa na **asilimia 104.2.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,746,197,542** ni “Retention”, **Shilingi 29,366,612** ni mishahara na **Shilingi 79,636,110** kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi.

## PROGRAMU KUU PL0203: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

**58.** **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inahusika na uimarishaji wa mazingira bora ya utendaji kazi wa Wizara, uratibu na usimamizi wa mipango. Programu hii ina Programu Ndogo tatu (3) ambazo

ni Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SL020301), Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti (SL020302) na Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Uchumi wa Buluu Pemba (SL020303).

59. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Kuu hii ilipangiwa **Shilingi 3,664,900,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,314,900,000** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 1,350,000,000** kwa matumizi mengineyo (OC). Hadi kufikia Machi 2026, Programu hii imepatiwa **Shilingi 2,290,910,603** sawa na **asilimia 62.5** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,679,042,822** ni Mishahara na **Shilingi 611,867,781** kwa ajili ya matumizi mengineyo ambayo sawa na **asilimia 45.3 (Kiambatanisho nambari 2).**

**i. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SL020301)**

60. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji inahusika na usimamizi wa rasilimali za Wizara, uimarishaji wa mazingira ya kufanyia kazi na utoaji wa huduma za kila siku za Wizara ambapo programu hii inahudumia jumla ya wafanyakazi 290 kwa Unguja na Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo: -

a) Imewajengea uwezo watumishi 16 kwa kuwapitia mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali

ndani na nje ya nchi na watumishi 28 kwa mafunzo ya muda mfupi katika maeneo mbalimbali ikiwemo ukuzaji wa mnyororo wa thamani kwa matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi. Aidha, watumishi 11 walipatiwa mafunzo elekezi ya awali (Orientation Course) na watumishi 235 walipatiwa mafunzo kuhusu utekelezaji wa programu mtambuka zinazohusiana na Usalama na Afya Kazini **(Kiambatanisho nambari 6 na 7).**

b) Imeimarisha mifumo ya Kiutumishi na Utendaji wa Wizara kwa kuandaa na kusimamia Mpango wa Rasilimali Watu (HRP), Mpango wa Urithishaji wa Uongozi (Succession Plan), Mpango wa Mafunzo, Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Customer Service Charter), pamoja na Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo (TNA).

c) Imekamilisha uandaaji wa Tovuti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa lengo la kutoa taarifa za utendaji kazi wa Wizara. Aidha, Wizara imetoa taarifa 50 kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kama vile twitter, fecebook na Instagram.

61. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa **Shilingi 1,800,000,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,000,000,000** ni Mishahara na **Shilingi 800,000,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufikia Machi

2026, programu hii imepatiwa **Shilingi 1,468,457,488** sawa na **asilimia 81.6** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 970,015,982** ni mishahara na **Shilingi 498,441,506** ni matumizi ya uendeshaji wa Ofisi sawa na **asilimia 62.3.**

**ii. Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti (SL020302).**

**62.** **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ina lengo la kusimamia utekelezaji wa mipango, miradi ya maendeleo na bajeti ya Wizara. Katika kipindi cha Julai – Machi cha mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Ndogo hii imetekeleza shughuli zifuatazo: -

a) Imeratibu uandaaji wa Sheria mpya ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari Zanzibar yenye lengo la kuimarisha usimamizi bora na endelevu wa matumizi ya rasilimali za uvuvi. Sheria hiyo itapelekea kufutwa kwa Sheria ya Uvuvi nambari 7 ya mwaka 2010 ambapo hatua iliyofikiwa ni kuwasilishwa Mswada wa Sheria hiyo katika Baraza la Wawakilishi. Vile vile, imeratibu tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2016 kwa lengo la kufanyiwa mapitio ya Sera hiyo ili kuvutia wawekezaji.

b) Imeratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi inayoendelea kutekelezwa na wizara pamoja

na kuandaa Ripoti ya Ufuatiliaji wa miradi ya Maendeleo kwa Robo tatu ya Mwaka (Julai hadi Machi 2025/2026) na kuiwasilisha Tume ya Mipango.

c) Imeendelea kukusanya na kusambaza takwimu za Sekta za Uchumi wa Buluu zinazohusiana na uzalishaji wa samaki, mwani na usafirishaji wa mazao ya baharini kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS).

d) Imeandaa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya wizara kwa kipindi cha robo mwaka, nusu mwaka na miezi tisa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2025-2030. Taarifa na ripoti hizo zimewasilishwa katika Mamlaka husika ikiwemo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Kamati ya Uchumi na Uwekezaji ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Tume ya Mipango.

e) Imeandaa Mpango wa Utekelezaji wa miaka mitano (5) wa Wizara kwa kuzingatia ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi alizozitoa katika kipindi cha kampeni za uchaguzi 2025, maagizo ya Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa Baraza la 12 la Wawakilishi 2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025-2030, Dira ya Maendeleo ya

2050 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP).

63. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa **Shilingi 470,000,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 190,000,000** ni Mishahara na **Shilingi 280,000,000** ni matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2026, Programu hii imepatiwa **Shilingi 174,979,276** sawa na **asilimia 37.2.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 127,450,550** ni mishahara na **Shilingi 47,528,726** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**iii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Uchumi wa Buluu Pemba (SL020303).**

64. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo hii ina jukumu la Karatibu shughuli zote zinazotekelezwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa upande wa Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo: -

a) Imetoa uelewa kwa wananchi 1,100 (Wanawake 470 na Wanaume 630), Vyuo vikuu 10 na Kamati za Uvuvi 8, kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za bahari, maendeleo ya Uchumi wa Buluu na Fursa zinazopatikana katika uchumi wa Buluu na Uvuvi.

b) Imewapatia mafunzo wafugaji 100 wa mazao ya baharini juu ya uanzishaji wa Jumuiya za

Wafugaji kwa lengo la kuchochea maendeleo ya Wafugaji hao.

c) Imetoa jumla ya leseni 2,168 kwa vyumbo vya uvuvi ili kuweza kuwatambua na kuimarisha huduma katika sekta ya uvuvi.

d) Imeendesha Doria 43 katika maeneo ya hifadhi ya PECCA kwa lengo la kudhibiti Uvuvi haramu. Aidha,Doria hizo zilihusisha Kamati za Uvuvi, Taasisi ya Blue Alliance, KMKM na Police Marine.

e) Imesajili wajasiriamali 60 wa uchakataji wa bidhaa za mwani katika mfumo maalum wa kanzi data (Database) ya Ofisi kwa lengo la kuwatambua, kuwapatia mafuzo na fursa mbalimbali kwa lengo la kuboresha bidhaa zao na kuinua kipato cha wajasiriamali hao.

f) Imetoa mafunzo ya uhamasishaji juu ya uazishwaji wa Hifadhi za muda mfupi za baharini kwa Kamati 49 za Uvuvi. Aidha, shehia 8 zimepatiwa elimu ya uhifadhi na kufuatilia viumbe vilivyopo hatarini kutoweka. Shehia hizo ni Makangale, Fundo, Junguni, Ukunjwi, Tondooni, Chambani, Shamiani na Muambe.

g) Imewajengea uwezo watumishi 57 kwa kuwapatia mafunzo kuhusu Sheria na Kanuni za Utumishi Serikalini kwa lengo kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi.

**65. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Uchumi wa Buluu Pemba iliidhinishiwa **Shilingi 1,394,900,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,124,900,000** ni Mishahara na **Shilingi 270,000,000** kwa Matumizi mengineyo (OC). Hadi kufikia Machi 2026, Programu Ndogo hii imepatiwa jumla ya **Shilingi 647,473,839** sawa na **asilimia 46.4.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 581,576,290** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 65,897,549** kwa matumizi mengineyo.

## E. CHANGAMOTO

**66. Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Changamoto zilizojitokeza ni kama zifuatazo:

i. Mwamko mdogo kwa Wananchi katika kuhifadhi na kutumia rasilimali za Bahari na fursa zinazotokana na Sekta za Uchumi wa Buluu.

ii. Uwepo wa vitendo vya uvuvi haramu pamoja na athari za mabadiliko ya Tabianchi, ambavyo vinaathiri upatikanaji endelevu wa rasilimali za bahari.

iii. Uhaba wa wataalamu katika sekta za Uvuvi, Uhifadhi wa bahari na Mafuta na Gesi Asilia.

**67. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeendelea kuchukua hatua zifuatazo:-

i. Inaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia semina, mikutano ya kijamii na vyombo vya habari ili kuongeza uelewa kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za bahari na fursa zilizopo katika Uchumi wa Buluu. Aidha, juhudi za kuimarisha mifumo ya usimamizi, sera na sheria zinazolenga uhifadhi wa rasilimali za bahari zimeendelea kuimarishwa.

ii. Imeimarisha doria za baharini, usimamizi wa sheria na mifumo ya udhibiti wa shughuli za uvuvi haramu. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu athari za mabadiliko ya Tabianchi na kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za uvuvi ambazo ni rafiki kwa mazingira.

iii. Imeendelea kuwajengea uwezo watumishi kupitia mafunzo ya kitaalamu ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

## F. MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**68. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Fungu la Bajeti 013 itaendelea kutekeleza

Programu Kuu tatu (3) na Programu Ndogo saba (7). Programu hizo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 zitakuwa zinajulikana kama ifuatavyo:

i. Programu Kuu P01: Maendeleo ya Uchumi wa Buluu ambayo imegawika katika;
   - Programu Ndogo S0101: Uratibu na Maendeleo ya Uchumi wa Buluu;
   - Programu Ndogo S0102: Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia;

ii. Programu Kuu P02: Maendeleo ya Uvuvi ambayo imegawika katika;
   - Programu Ndogo S0201: Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini;
   - Programu Ndogo S0202: Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari

iii. Programu Kuu P03: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ambayo imegawika katika;
   - Programu Ndogo S0301:Utumishi na Uendeshaji;
   - Programu Ndogo S0302: Mipango, Sera na Utafiti;
   - Programu Ndogo S0303: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Uchumi wa Buluu na Uvuvi – Pemba;

## VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

69. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza programu hizo, Wizara ina vipaumbele vinne (4) ambavyo ni:

i. Kuimarisha uvuvi wa bahari kuu kwa kufanya ununuzi wa meli za uvuvi wa bahari kuu, ujenzi wa viwanda vya kuchakata samaki sambamba na uanzishaji wa Eneo huru la Uwekezaji wa Uchumi wa Buluu – Fungurefu.

ii. Kuendeleza Uvuvi Mdogo Mdogo kwa kufanya ujenzi wa madiko na masoko ya kisasa ya samaki, kuanzisha maabara ya kisasa kwa ajili ya kuthibitisha mazao ya baharini katika soko la ndani na la nje pamoja na kuimarisha ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba.

iii. Kulipa hadhi zaidi zao la mwani kwa kujenga viwanda vidogo vidogo na vikubwa vya kibiashara ili kusarifu zao hilo na kuongeza thamani pamoja na kuendelea kuwawezesha wakulima wa mwani kwa kuwapatia pembejeo na elimu iliyo bora ili kuongeza uzalishaji.

iv. Kuimarisha sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa kufanya utafiti wa utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa njia ya mtetemo ya 2D na 3D pamoja na kujenga Kituo cha Kudumu cha kuhifadhia Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR).

## MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**70.** **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza programu na vipaumbele hivyo, kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza Miradi kumi (10) ya maendeleo yenye thamani ya **Shilingi 193,242,710,000.** Miradi hiyo ni: -

i. Mradi wa ujenzi wa viwanda vya kuchakata Samaki na uzalishaji wa malighafi.

ii. Mradi wa uanzishwaji wa eneo Huru la Uwekezaji wa Uchumi wa Buluu (Fungurefu).

iii. Mradi wa Maendeleo Endelevu ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini – TASFAM.

iv. Mradi wa kuendeleza Uvuvi na Kilimo – AFDP (IFAD).

v. Mradi wa Uendelezaji na uanzishwaji wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki.

vi. Mradi wa Uanzishwaji wa Maabra ya ZAFIRI kwa Bidhaa za Uvuvi na Ufugaji wa Viumbe Maji na Kulipa hadhi zao la mwani.

vii. Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini.

viii. Mradi wa Mashirikiano wa Kulinda na Kusimamia Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani katika eneo la Bahari ya Hindi Magharibi.

ix. Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Uhifadhi wa Data za Mafuta na Gesi Asilia (NDR), na

x. Mradi wa Uchukuaji wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia kwa njia ya Mtetemo wa 3D (3D Seismic Survey).

Mheshimiwa Spika, Mchanganuo wa Fedha za Utekelezaji wa Miradi hiyo unafafanuliwa katika **Kiambatanisho nambari 3.**

**71.** **Mheshimiwa Spika,** Mipango yote ya utekelezaji wa Malengo hayo yaliyowekwa na Wizara, umezingatia masuala ya kijinsia kwa lengo la kuendelea kutekeleza Mkakati wa Ukondoishaji wa Masuala ya Kijinsia katika Uchumi wa Buluu (Gender Mainstreaming Strategy in the Blue Economy) pamoja na Mpango Kazi wake wa mwaka 2023.

## G. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA PROGRAM KUU PO1: MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

### Programu Ndogo ya Uratibu na Maendeleo ya Uchumi wa Buluu (S0101)

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Programu Ndogo ya Uratibu na Maendeleo ya Uchumi wa Buluu (S0101) inayotekelezwa na Idara ya Uratibu wa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

a) Kusimamia uanzishwaji wa Eneo Huru la Uwekezaji wa Uchumi wa Buluu na kulipanga

kimatumizi “Master Plan” katika eneo la Fungurefu kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi kwa uwekezaji na kuchochea ukuaji wa Uchumi wa Buluu.

b) Kuendelea kupanga Mpango wa Matumizi ya Bahari (MSP) na kuratibu ushirikiano wa sekta na taasisi zinazotekeleza Sera ya Uchumi wa Buluu kwa lengo la kuhakikisha matumizi bora ya maeneo ya bahari.

73. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Ndogo hii iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya **Shilingi 5,422,467,300.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 100,307,100** kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 322,160,200** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 5,000,000,000** ni fedha za utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo kutoka SMZ **(Kiambatanisho nambari 4).**

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia (S0102)**

74. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo hii (S0102) inahusisha Usimamizi wa Shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC). Wizara kupitia Programu Ndogo hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

**i. Malengo yatakayotekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia.**

a) Kuimarisha mfumo wa kisera kwa kufanya mapitio ya Sera ya Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2016 ili kuvutia wawekezaji.

b) Kuratibu shughuli za uchukuaji wa Taarifa (Data) za Mafuta na Gesi Asilia kwa njia ya Mtetemo (2D na 3D seismic surveys) kwa maeneo ya nchi kavu na baharini ili kupata taarifa muhimu na za uhakika kitaalamu kwa ajili ya kujua maeneo ya kuchimba visima na kuvutia wawekezaji.

c) Kuendelea na utangazaji wa Vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia kwa lengo la kuvutia wawekezaji, pamoja na kuendelea na majadiliano ya mikataba ya mgawanyo wa uzalishaji wa mafuta na gesi asilia (PSA) na Kampuni za Mafuta na Gesi Asilia.

d) Kuelimisha jamii kuhusu shughuli za mafuta na gesi asilia kwa lengo la kuhamasisha ushiriki wa wananchi na kutambua fursa za kiuchumi zinazotokana na Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

e) Kuzijengea uwezo Taasisi za Mafuta na Gesi Asilia katika usimamizi wa sekta kwa lengo la kuimarisha uwezo wa usimamizi wa shughuli za Mafuta na Gesi Asilia.

### ii. Malengo yatakayotekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA).

a) Kusimamia shughuli za ukusanyaji wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia pamoja na Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia zitakazofanywa na Kampuni za Mafuta na Gesi Asilia kwa kuzingatia mikataba yao na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

b) Kuendelea kuimarisha miundombinu ya kisasa ya usimamizi na uhifadhi wa taarifa za mafuta na gesi asilia kupitia ZPRA kwa kujenga Kituo Maalumu cha Kudumu cha Kuhifadhi Taarifa (NDR) na sampuli za mafuta na gesi asilia pamoja na ununuzi wa vifaa vya kuchakata na kuhifadhia Taarifa.

c) Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi wa Mamlaka ikiwemo ubora wa ofisi, nguvu kazi na maslahi ya watendaji pamoja na kuwajengea uwezo watendaji waliopo ili kuchochea uwajibikaji wao na kuongeza ufanisi.

### iii. Malengo yatakayotekelezwa na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta Na Gesi Asilia (ZPDC).

a) Kuchukua, kuchakata na kutafsiri (3D data acquisition, prosessing and interpretation) taarifa za mafuta na Gesi asilia kwa maeneo ya Kinyasini na Paje.

b) Kufanya uwekezaji kupitia ZPDC katika mkondo wa chini wa shughuli za mafuta na gesi asilia kwa lengo la kutanua wigo wa kibiashara kwa Kampuni.

c) Kuwajengea uwezo wataalamu wa ZPDC kwa utekelezaji wa shughuli za utafutaji wa taarifa za mafuta na gesi asilia pamoja na uchimbaji wa visima.

75. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Ndogo ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia (S0102) iweze kutekeleza malengo yaliyopangwa kwa ufanisi, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 49,602,190,700.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 305,000,000** kwa Kazi za Kawaida za Idara ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia, **Shilingi 79,980,700** ni Mishahara kwa ajili ya Idara ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia, na **Shilingi 3,217,210,000** ni ruzuku kwa ajili ya Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA). Aidha, katika kutelekeza Miradi ya Maendeleo, Programu Ndogo hii inaombewa jumla ya **Shilingi 46,000,000,000.**

76. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (P01) iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 55,024,658,000** ambapo **Shilingi 2,067,117,800** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi**

**1,957,540,200** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 51,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo **(Kiambatanisho nambari 4).**

## H. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA PROGRAMU KUU P02: MAENDELEO YA UVUVI

### Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini (S0201)

**77. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini (S0201) inayotekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI), Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) na Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

#### i. Malengo yatakayotekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini

**78. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

a) Kuanzisha kituo maalum cha Serikali cha uuzaji wa zana za uvuvi kwa lengo la kuwapatia wavuvi wadogo wadogo unafuu wa upatikanaji wa vitendea kazi.

b) Kuendelea kuwapatia vifaa na elimu wavuvi na wakulima wa mwani ikiwemo boti ili kuongeza uzalishaji na kujipatia kipato.

c) Kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya uvuvi ili kuimarisha mnyororo wa thamani kwa kujenga madiko ya kisasa kwa Unguja na Pemba ikiwemo maeneo ya Kizimkazi, Unguja Ukuu, Nungwi, Kigomani, Tumbatu, Wete, Mtambwe, Kichuwani na Kojani. Aidha, Wizara inaendelea na ukamishaji wa ujenzi wa madiko matano (5) ya kisasa katika maeneo ya Fukuchani, Pitanazako, Kengeja, Kiwani na Msuka.

d) Kujenga ghala ya kuhifadhia shehena za dagaa kwa ajili ya kusafirisha, kujenga vizimba vya kufugia samaki kwa mfumo wa kuimarisha ukulima na ufugaji baharini (Mariculture), kujenga miundombinu ya baridi (cold room) na kufunga mitambo ya kisasa ya kuzalisha barafu (ice plants) katika madiko kwa Unguja na Pemba.

e) Kuanza rasmi ujenzi wa viwanda vya kisasa vya kuchakata samaki (fish processing plants) kwa Unguja na Pemba kwa lengo la kuongeza thamani ya rasilimali ya samaki, kuinua kipato cha wavuvi na kuongeza bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi ili kuongeza pato la fedha za kigeni.

f) Kuendeleza ujenzi wa Kiwanda cha kusarifu dagaa kilichopo Ndagoni kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa soko la uhakika kwa wanaojishughulisha na shughuli za dagaa na kuiongezea hadhi bidhaa ya dagaa ili kuingia katika soko la ushindani.

g) Kuimarisha sekta ya uvuvi kupitia matumizi ya mifumo ya kisasa (digitalization) kwa kuwasajili wavuvi, wakulima wa mwani na wafugaji wa viumbe maji na kuwapatia vitambulisho vya kisasa vya kielektroniki ili waweze kutambulika na kupata huduma kadhaa ikiwemo huduma ya bima na huduma za kifedha ikiwemo mikopo kupitia taasisi za kifedha.

h) Kuanza hatua za maandalizi ya ujenzi wa chuo cha uvuvi kitakachotoa mafunzo ya uvuvi hadi ngazi ya Diploma kwa lengo la kutanua wigo wa uelewa wa uvuvi wa kisasa unaoendana na dunia ya leo.

i) Kufanya sensa ya mnyororo wa thamani katika sekta ya uvuvi kwa lengo la kutambua idadi ya wavuvi, wakulima wa mwani, wafugaji wa viumbe maji na wasarifu wa mazao ya baharini ili kuweza kupanga mikakati bora zaidi ya sekta husika.

j) Kuimarisha usalama wa wavuvi kwa kuwapatia vifaa vya uokozi na mawasiliano, kuwapa mafunzo ya usalama baharini pamoja na kuimarisha usimamizi wa usajili wa vyombo vya uvuvi.

k) Kurasimisha zao la chumvi ili kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa soko la zao la chumvi kama sehemu ya mazao ya baharini kwa wanaojishughulisha na zao hilo.

l) Kujenga kituo kikubwa cha kisasa cha kufundishia namna bora ya kusarifu mwani na majongoo bahari

katika eneo la Chokochoko, Pemba, kwa lengo la kuongeza thamani ya mazao hayo, kuimarisha ushindani wa bidhaa katika masoko ya ndani na nje ya nchi, kuchochea ajira na kuongeza kipato kwa wakulima wa mwani na wafugaji wa majongoo bahari.

m) Kujenga ghala za kuhifadhia mwani ili kupata mwani uliohifadhiwa kwa ubora na kuweza kuingia katika ushindani wa soko la Kimataifa kwa vigezo vinavyokubalika.

n) Kujenga viwanda vya kusarifu mwani ili kupata bidhaa bora za mwani kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi na kutanua wigo wa kupatikana ajira pamoja na kuongeza fursa za kipato kwa wananchi wanaojishughulisha na shughuli za ukulima wa mwani.

o) Kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari Zanzibar kwa lengo la kusimamia, kuendeleza na kuratibu matumizi endelevu ya rasilimali za Uvuvi Zanzibar.

p) Kuimarisha upatikanaji wa vitendea kazi kwa lengo la kujenga ufanisi bora kwa Wizara na Taasisi zake ikiwemo magari, boti za kisasa za doria na magari maalumu ya mitambo ya barafu kwa ajili ya kuhifadhia mazao ya baharini ikiwemo Samaki.

ii. **Malengo yatakayotekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Baharini (ZAFIRI)**

79. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZAFIRI imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

a) Kuendeleza shughuli za tafiti za uvuvi na kutoa matokeo ya tafiti kwa lengo la kuimarisha matumizi ya tafiti ili kupata matokeo chanya katika usimamizi wa rasilimali za baharini.

b) Kuendelea kuimarisha maabara ya ZAFIRI katika kufanya tafiti na matumizi ya tafiti hizo ili kuendeleza ukulima wa mwani na ufugaji wa samaki na viumbe maji wengine.

c) Kujenga kituo cha kisasa cha kuzalisha mbengu bora za mwani zenye uhimilivu wa mabadiliko ya Tabianchi ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa mbegu za mwani na kuongeza uzalishaji wa mwani nchini.

d) Uthaminishaji (Accreditation) wa Mazao ya baharini katika viwango vya kimataifa (ISO standards) ili kupata bidhaa zinazotokana na mazao ya baharini zenye uthibitisho wa alama ya ubora unaokubalika Kimataifa na kuweza kuingia katika soko la Kimataifa.

iii. **Malengo yatakayotekelezwa na Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO)**

80. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZAFICO imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

a) Kujenga bandari ndogo ya Uvuvi (Wharf) katika eneo la Malindi kwa lengo la kuimarisha uvuvi wa bahari kuu.

b) Ununuzi wa meli kubwa za kisasa za uvuvi wa bahari kuu kwa lengo la kuendeleza jitihada za uvuvi wa Bahari kuu na kuongeza kiwango cha samaki wanaovuliwa Zanzibar.

c) Kuimarisha biashara ya uuzaji wa Samaki na dagaa kwa ubora unaokubalika katika soko la ndani na soko la Kimataifa.

iv. **Malengo yatakayotekelezwa na Kampuni ya Mwani ya Serikali (ZASCO)**

81. **Mheshimiwa Spika,** napenda nilitaarifu Baraza lako Tukufu kwamba, kwa kuwa zao la mwani ni miongoni mwa mazao muhimu ya baharini, na kwa lengo la kulipa hadhi zaidi zao hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya maamuzi ya makusudi kuihamisha Kampuni ya Mwani (ZASCO) kutoka Wizara ya Biashara na Viwanda kuja katika Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuanzia mwaka huu wa fedha 2026/2027. Kwa mantiki hiyo, Wizara kupitia ZASCO imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

a) Kukizindua rasmi kiwanda cha Mwani Chamanangwe kwa kuhakikisha miundombinu na mitambo inakamilika na kuanza kazi.

b) Kuanza ununuzi wa mwani ghafi kupitia Kiwanda cha mwani cha Chamanangwe kwa lengo la kuweka soko la uhakika kwa wakulima wa mwani.

c) Kuendeleza taratibu za ukamilishwaji wa Kiwanda kipya cha kuchakata mwani kinachotarajiwa kujengwa kwa ubia kati ya Kampuni ya ZASCO na Kampuni binafsi.

d) Kuimarisha upatikanaji wa soko la mwani kwa ndani na nje ya nchi kwa kuanzisha vituo maalumu vya kununulia mwani katika kila Wilaya kwa lengo la kurahisisha huduma za uuzaji wa mwani kwa wakulima wa mwani.

e) Kuurasimisha rasmi mwani aina ya Ulva unaopatikana katika fukwe nyingi za bahari na katika kiwango kikubwa kwa lengo la kuongeza fursa za ajira kwa wananchi wanaojishughulisha na kilimo cha mwani.

f) Kuzipitia na kuzitathmini upya bei za mwani unaotokana na ukulima wa mwani ili kuendana na thamani ya jitihada za wakulima wa mwani.

g) Kuwekeza katika miundombinu ya mnyororo wa thamani ikiwemo ujenzi wa makaushio, maghala ya kuhifadhia mwani na vituo vya kupimia na kununua

mwani Unguja na Pemba, pamoja na ununuzi wa magari ya usafirishaji ili kupunguza upotevu na kuongeza ubora wa mwani.

h) Kuwawezesha wakulima wa mwani kwa kuwapatia vifaa vya kisasa vya kilimo cha mwani pamoja na mbegu bora kwa lengo la kuongeza uzalishaji, kuboresha ubora wa mwani na kuongeza kipato cha wakulima wa mwani.

**v. Malengo yatakayotekelezwa na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA)**

**82. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha usimamizi endelevu wa bahari kuu, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

a) Kutoa leseni na vibali kwa meli za uvuvi wa bahari kuu kwa lengo la kudhibiti na kusimamia shughuli za uvuvi wa bahari kuu na kuongeza mapato yatokanayo na uvuvi wa bahari kuu kwa Serikali.

b) Kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (EEZ) kwa kuboresha mifumo ya ufuatiliaji na uangalizi wa meli za uvuvi (Vessels Monitoring System – VMS Automatic Identification System – AIS) kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu, usioripotiwa na usiodhibitiwa (IUU Fishing).

c) Kuendelea kuwezesha na kuratibu tafiti katika bahari kuu kwa ajili ya kuimarisha uhifadhi, usimamizi, udhibiti na uendelezaji wa uvuvi wa bahari kuu.

83. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Bahari iweze kutekeleza kazi zake ipasavyo, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya **Shilingi 147,542,472,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,166,634,000** kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi 1,518,638,100** ni Mishahara kwa ajili ya Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, **Shilingi 927,840,140** ni Matumizi mengineyo ya Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, **Shilingi 720,155,760** ni Mishahara ya Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO). Aidha, **Shilingi 2,133,129,000** ni ruzuku kwa Taasisi zinazojitegemea ambapo **Shilingi 1,448,189,000** ni ruzuku kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI) na **Shilingi 684,940,000** ni ruzuku ya Mishahara kwa ajili ya Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO).

84. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Programu Ndogo hii inaombewa **Shilingi 142,242,710,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 79,255,390** kutoka SMZ na **Shilingi 62,987,320,00**0 ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo **(Kiambatanisho nambari 4).**

### Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari (S0202)

85. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari (S0202) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

a) Kuimarisha maeneo mawili (2) mapya ya uhifadhi Mashariki mwa Kisiwa cha Pemba (Kusini Mashariki na Kaskazini Mashariki), kuendeleza uhifadhi wa Bioanuai na Rasilimali za Baharini pamoja na Udhibiti wa Viumbe waliohatarini kutoweka.

b) Ununuzi wa boti saba (7) za kisasa zenye nyezo zote zinazohitajika kwa ajili ya doria za maeneo ya hifadhi.

c) Kuimarisha Miundombinu ya Maeneo ya Hifadhi kwa ujenzi wa ofisi mbili (2) za maeneo ya hifadhi, vituo vya doria na vituo maalumu vya utoaji wa taarifa za uhifadhi (information centers). Jitihada zote zinazofanywa na Idara ya Uhifadhi zinalenga kuimarisha Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Bahari na Jamii zilizozunguka maeneo ya Hifadhi za Bahari ikiwemo kuimarisha Kamati za kijamii za hifadhi kwa lengo la kuongeza mapambano dhidi ya uvuvi haramu na uharibifu wa Hifadhi za bahari.

86. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Ndogo hii iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya

**Shilingi 3,070,333,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 140,467,350** ni Mshahara na **Shilingi 230,000,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 2,699,865,650** ni "Retention" ya Makusanyo ya Idara ya Uhifadhi.

87. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi (P02) iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 150,612,806,000** ambapo **Shilingi 4,097,630,210** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 4,272,465,790** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 142,242,710,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## I. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA PROGRAM KUU PO3: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

### Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji (S0301)

88. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi wa Wizara na kuhakikisha utoaji wa huduma bora na zenye tija, Wizara kupitia Programu Ndogo hii inayotekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

a) Kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi ya Wizara kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu.

b) Kuendeleza na kusimamia rasilimali watu kwa tija kupitia programu endelevu za kujenga uwezo wa watumishi kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa lengo la kuongeza ujuzi, weledi na tija kazini.

c) Kuimarisha mifumo ya utoaji huduma na mawasiliano ya Wizara kwa kuboresha huduma kwa wateja kupitia utekelezaji madhubuti wa mikataba ya huduma kwa lengo la kuongeza ubora wa huduma na kuridhika kwa wateja.

d) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA, huduma za Kisheria na uwazi katika utoaji wa taarifa kwa umma kwa lengo la kuongeza uwajibikaji, upatikanaji wa taarifa sahihi na kuimarisha imani ya wananchi kwa Wizara.

**89.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha kwamba Programu Ndogo hii inatekeleza malengo yake ipasavyo, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya **Shilingi 1,761,919,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,161,119,266** ni Mishahara na **Shilingi 600,799,734** kwa matumizi mengineyo.

**Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti (S0302)**

**90.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuratibu kazi za Mipango Sera na Utafiti kwa maendeleo ya sekta za Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Wizara kuptitia Programu Ndogo hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

a) Kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo ya Wizara, kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wake kwa lengo la kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa ufanisi na kutoa matokeo chanya.

b) Kuandaa tafiti mbali mbali za Wizara kwa mujibu wa agenda ya Utafiti ya Zanzibar kwa lengo la kusaidia kufanya maamuzi ya kisera na mipango ya maendeleo ya Wizara.

c) Kuratibu na kuandaa Miongozo ya Kisera na Kisheria, Mipango, Bajeti pamoja na ripoti za utekelezaji wa kazi za Wizara kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Wizara.

91. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya **Shilingi 493,863,000** kwa ajili ya Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 193,769,100** ni Mishahara na **Shilingi 300,093,900** ni matumizi mengineyo.

**Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Uchumi wa Buluu na Uvuvi - Pemba (S0303)**

92. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo hii inahusiana na utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa upande wa Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara kupitia Programu Ndogo hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

a) Kuendelea kuimarisha uratibu wa shughuli zote za Wizara kwa Pemba kwa lengo la kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Wizara.
b) Kuimarisha doria za baharini kwa upande wa Pemba kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu na kulinda rasilimali za bahari.
c) Kuendeleza programu za elimu kwa jamii katika Wilaya zote za Pemba kupitia mikutano na vyombo vya habari kwa lengo la kuongeza uelewa na kuhamasisha ushiriki wa jamii katika usimamizi, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

**93.** **Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza kazi za Wizara kupitia Programu Ndogo hii, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya **Shilingi 1,114,253,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 888,252,624** ni Mishahara na **Shilingi 226,000,376** kwa matumizi mengineyo.

**94.** **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (P03) iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 3,370,035,000** ambapo **Shilingi 2,243,140,990** kwa ajili ya mishahara, na **Shilingi 1,126,894,010** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

## J. MAOMBI YA KUIDHINISHIWA MAPATO NA MATUMIZI KWA FUNGU LA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI (013) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**95.** **Mheshimiwa Spika,** ili Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iweze kutekeleza malengo na mipango iliyokusudiwa, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama ifuatavyo;

**96.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kuidhinishiwa matumizi ya **Shilingi 209,007,499,000** kwa **Fungu la Bajeti 013** ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,764,789,000** kwa Kazi za Kawaida, ambapo **Shilingi 4,802,690,000** ni mishahara, **Shilingi 5,611,760,000** ni matumizi ya uendeshaji wa ofisi (OC) na **Shilingi 5,350,339,000** ni ruzuku ya Mishahara na kazi za kawaida (OC) kwa Taasisi zinazojitigemea. Kati ya fedha za ruzuku za Taasisi zinazojitegemea, **Shilingi 3,217,210,000** ni ruzuku ya mshahara na kazi za kawaida kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA), **Shilingi 1,448,189,000** ni ruzuku ya mshahara na kazi za kawaida kwa Taasisi ya Uvuvi na Maliasili za Bahari (ZAFIRI) na **Shilingi 684,940,000** ni ruzuku ya Mshahara kwa Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO). **(Kiambatanisho nambari 4).**

97. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kazi za Maendeleo, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha **Shilingi 193,242,710,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 130,255,390,000** ni fedha za SMZ na **Shilingi 62,987,320,000** ni fedha za Wahisani (Mkopo ni **Shilingi 58,910,954,775** na ruzuku ni **Shilingi 4,076,365,225) (Kiambatanisho nambari 3 na 4).**

98. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 13,251,303,000** ikiwa ni mapato yatakayokusanywa kupitia vyanzo vya Makusanyo **(Kiambatanisho nambari 5)**

99. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuidhinishiwa matumizi ya **Shilingi 25,000,000,000** kwa Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO) ikiwa ni mtaji wa kutekeleza shughuli za Kampuni ambapo mapato na matumizi yatasimamiwa na Mkurugenzi Mkuu wa ZASCO.

100. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, naomba kuidhinishiwa matumizi ya **Shilingi 3,000,000,000** kwa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) ikiwa ni fedha za kutekeleza shughuli za Kampuni ambapo matumizi yake yatasimamiwa na Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZPDC.

## K. SHUKRANI

101. **Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wa kipekee natoa shukurani zangu za dhati kwa Tume ya Mipango Zanzibar inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Viongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango chini ya usimamizi mzuri wa Mheshimiwa Waziri Dkt. Juma Malik Akil na wasaidizi wake pamoja na Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Dkt. Afua Khalfan Mohammed. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Talib Haji Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kwa ushauri wa kisheria katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

102. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kutumia fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa misaada na michango yao katika kuchangia maendeleo ya kitaifa kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Miongoni mwa Washirika hao ni pamoja na; Benki ya Dunia (World Bank) inayofadhili mradi wa Maendeleo Endelevu ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini (TASFAM), Mfuko wa Kimataifa ya Maendeleo ya Kilimo (IFAD) unaofadhili mradi wa Kuendeleza Uvuvi na Kilimo, Shirika la Chakula Duniani (FAO), Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Japan (JICA) na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA). Vile vile natoa shukurani kwa Jumuiya ya Chama Cha Sayansi ya Bahari ya Hindi ya Magharibi (WIOMSA),

Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira (TNC), Mfuko wa Dunia wa Hifadhi ya Asili na Wanyamapori (WWF), Jumuiya ya Uhifadhi Duniani (WCS), Marine Cultures, Milele Foundation, Mwambao, Blue Alliance na Umoja wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Asili (IUCN) katika utekelezaji wa programu za utafiti, uwezeshaji na uhifadhi wa bahari. Aidha, napenda kutoa shukuruni za kipekee kwa Jumuiya zisizo za Kiserikali (NGOs) ikiwemo Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF) pamoja na Washirika wote ambao sikuweza kuwataja hapa.

103. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wenzetu wanaojishughulisha na uvuvi, ukulima wa mwani, wafugaji wa mazao ya baharini na wanakamati za hifadhi za uvuvi kwa mashirikiano yao makubwa wanayoyatoa kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi pamoja na kazi yao kubwa wanayoifanya katika kuendeleza na kuimarisha uvuvi, uhifadhi wa rasilimali na ufugaji wa mazao ya baharini ambao umetoa mchango mkubwa kwa Taifa.


104. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru watendaji wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Taasisi zilizo chini yake kwa kufanya kazi kwa umahiri, weledi ufanisi na moyo wa uzalendo na kujitolea kwa maslahi mapana ya Zanzibar. Shukurani maalum nazitoa kwa Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Mboja Ramadhan

Mshenga Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mahonda kwa mashirikiano makubwa anayonipatia katika kuisimamia Wizara hii. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu, Kepteni Hamad Bakar Hamad, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Zahor Kassim Mohammed El Kharousy, Afisa Mdhamini, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi zote na Watumishi wote wa Wizara kwa mashirikiano makubwa wanayonipatia na kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

## L. HITIMISHO

105. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, nawaomba wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie hotuba hii, washauri ipasavyo na hatimae waipitishe Bajeti hii ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

106. **Mheshimiwa Spika,** nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.



.............................................................

**MHE. MASOUD ALI MOHAMMED (MBM)**
**WAZIRI WA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**
**ZANZIBAR**

# VIAMBATANISHO

## Kiambatanisho Nam. 1: Ukusanyaji Mapato kwa Kipindi cha Julai 2025 – Machi, 2026

| Fungu (Vote) | Chanzo cha Mapato | Makadirio ya Mapato 2025/2026 | Mapato Halisi Julai-Machi 2026 | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| LO2- PEMBA | LESENI ZA UVUVI | 55,725,865 | 19,309,000 | 35 |
| | ADA YA MAZAO BAHARINI | 128,598,150 | 36,900,655 | 29 |
| | TOZO ZA MADIKO | 8,577,210 | - | - |
| | ADA YA UINGIAJI WA WAGENI (PECCA) | 235,763,275 | 96,575,509 | 41 |
| | **JUMLA NDOGO** | **428,664,500** | **152,785,164** | **36** |
| LO2- UNGUJA | LESENI ZA UVUVI | 162,890,990 | 38,738,999 | 24 |
| | ADA YA MAZAO BAHARINI | 618,985,762 | 381,095,860 | 62 |
| | TOZO ZA MADIKO | 32,578,198 | - | - |
| | MAPATO YA UVUVI WA BAHARI KUU | 3,257,819,800 | 796,272,000 | 24 |
| | ADA YA UINGIAJI WA WAGENI (MENAI & MIMCA) | 6,772,274,750 | 7,124,311,449 | 105 |
| | **JUMLA NDOGO** | **10,844,549,500** | **8,340,418,308** | **77** |
| **JUMLA KUU** | | **11,273,214,000** | **8,493,203,472** | **75** |

## Kiambatanisho Nam. 2: Mchanganuo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Mwaka 2025/2026

| PROGRAMU | MAKADIRIO | UPATIKANAJI WA FEDHA ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2025/2026 | | | | | | JUMLA | ASILI MIA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MSHAHARA | MATUMIZI KAWAIDA | RUZUKU | | MIRADI | | | |
| | | | | MSHAHARA | KAWAIDA | SMZ | MHISANI | | |
| P01 Maendeleo ya Uchumi wa Buluu | 26,740,300,000 | 70,727,375 | 154,551,093 | 1,135,809,041 | 363,741,820 | 14,141,245,200 | | 15,866,074,529 | 59.3 |
| S0101 Maendeleo ya Uchumi wa Buluu | 7,201,500,000 | 70,727,375 | 113,555,438 | - | - | - | - | 184,282,813 | 2.6 |
| S0102 Maendeleo ya mafuta na Gesi | 488,000,000 | - | 40,995,655 | - | - | - | - | 40,995,655 | 8.4 |
| Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia | 10,050,800,000 | - | - | 1,135,809,041 | 363,741,820 | - | - | 1,499,550,861 | 14.9 |
| Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia | 9,000,000,000 | - | - | - | - | 14,141,245,200 | - | 14,141,245,200 | 157.1 |
| P02 Maendeleo ya Uvuvi | 141,628,761,377 | 1,191,552,587 | 3,959,247,598 | 939,296,525 | 77,052,188 | 8,742,845,339 | 2,049,176,284 | 16,959,170,521 | 12.0 |
| S0201 Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini | 136,358,861,377 | 1,162,185,975 | 133,413,946 | - | - | 8,614,474,427 | 2,049,176,284 | 11,959,250,632 | 8.8 |
| S0202 Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari | 1,200,000,000 | 29,366,612 | 79,636,110 | - | - | - | - | 109,002,722 | 9.1 |
| Fedha za Retention | 2,500,000,000 | - | 3,746,197,542 | - | - | - | - | 3,746,197,542 | 149.8 |
| Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini Zanzibar | 1,140,500,000 | - | - | 582,625,025 | 77,052,188 | - | - | 659,677,213 | 57.8 |
| Kampuni ya Uvuvi Zanzibar | 429,400,000 | - | - | 356,671,500 | | 128,370,912 | | 485,042,412 | 113.0 |
| P03 Uendeshaji na Uratibu wa Wizara | 3,664,900,000 | 1,679,042,822 | 611,867,781 | - | - | - | - | 2,290,910,603 | 62.5 |
| S0301 Utawala na Uendeshaji | 1,800,000,000 | 970,015,982 | 498,441,506 | - | - | - | - | 1,468,457,488 | 81.6 |
| S0302 Mipango, Sera na Utafiti | 470,000,000 | 127,450,550 | 47,528,726 | - | - | - | - | 174,979,276 | 37.2 |
| S0303 Uratibu wa kazi za Wizara Pemba | 1,394,900,000 | 581,576,290 | 65,897,549 | - | - | - | - | 647,473,839 | 46.4 |
| JUMLA | 172,033,961,377 | 2,941,322,784 | 4,725,666,471 | 2,075,105,566 | 440,794,008 | 22,884,090,539 | 2,049,176,284 | 35,116,155,652 | 20.4 |

## Kiambatanisho Nam. 3: Makadirio ya Fedha za Miradi ya Maendeleo 2026/2027

| NAM | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO 2026 - 2027 | | |
|---|---|---|---|---|
| | | SMZ | MUHISANI | JUMLA |
| | **PROGRAMU YA KUIMARISHA UVUVI WA BAHARI KUU** | | | |
| 1 | Mradi wa ujenzi wa viwanda vya kuchakata Samaki na uzalishaji wa malighafi | 39,000,000,000 | | 39,000,000,000 |
| 2 | Mradi wa uanzishwaji wa eneo Huru la Uwekezaji wa Uchumi wa Buluu (Fungurefu) | 5,000,000,000 | | 5,000,000,000 |
| 3 | Mradi wa Maendeleo Endelevu ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini - TASFAM | | 45,412,300,000 | 45,412,300,000 |
| 4 | Mradi wa kuendeleza Uvuvi na Kilimo - AFDP | | 13,498,654,587 | 13,498,654,587 |
| | **PROGRAMU YA KUENDELEZA WAVUVI WADOGO WADOGO** | | | |
| 5 | Mradi wa Uendelezaji na uanzishwaji wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki | 24,044,040,167 | | 24,044,040,167 |
| 6 | Mradi wa Uanzishwaji wa Maabra ya ZAFIRI kwa Bidhaa za Uvuvi na Ufugaji wa Viumbe Maji na Kulipa hadhi zao la mwani | 16,211,350,833 | | 16,211,350,833 |
| 7 | Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini | | 1,118,000,000 | 1,118,000,000 |
| 8 | Mradi wa Mashirikiano wa Kulinda na Kusimamia Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani katika eneo la Bahari ya Hindi Magharibi | | 2,958,365,000 | 2,958,365,000 |
| | **PROGRAMU YA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA MAFUTA NA GESI ASILIA** | | | |
| 9 | Mradi wa Uanzishaji Kituo cha Taifa cha Uhifadhi wa Data za Mafuta na Gesi Asilia | 11,000,000,000 | | 11,000,000,000 |
| 10 | Mradi wa Kufanya Utafiti wa Utafutaji wa Mafuta kwa njia ya Mtetemo wa 3D | 35,000,000,000 | | 35,000,000,000 |
| **JUMLA KUU** | | **130,255,391,000** | **62,987,319,587** | **193,242,710,587** |

## Kiambatanisho Nam. 4: Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

| PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | MAKADIRIO YA FEDHA ZA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2026/2027 | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MSHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU KAWAIDA | RUZUKU MISHAHARA | MAENDELEO | | | JUMLA |
| | | | | | SMZ | MHISANI | | |
| | | | | | SMZ | RUZUKU | MKOPO | |
| **P 01: Maendeleo ya uchumi wa Buluu** | **180,287,800** | **627,160,200** | **1,330,380,000** | **1,886,830,000** | **51,000,000,000** | | | **55,024,658,000** |
| S0101: Uratibu wa Uchumi wa Buluu | 100,307,100 | 322,160,200 | | | 5,000,000,000 | | | 5,422,467,300 |
| S0102: Maendeleo ya Mafuta na Gesi | 79,980,700 | 305,000,000 | | | 46,000,000,000 | | | 49,602,190,700 |
| Idara ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia | 79,980,700 | 305,000,000 | | | | | | 384,980,700 |
| ZPRA | | | 1,330,380,000 | 1,886,830,000 | 11,000,000,000 | | | 14,217,210,000 |
| ZPDC | | | | | 35,000,000,000 | | | 35,000,000,000 |
| **P02: Maendeleo ya Uvuvi** | **2,379,261,210** | **3,857,705,790** | **414,760,000** | **1,718,369,000** | **79,255,390,000** | **4,076,365,225** | **58,910,954,775** | **150,612,806,000** |
| S0201: Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini | 1,518,638,100 | 927,840,140 | - | - | 63,044,039,667 | 4,076,365,225 | 58,910,954,775 | 128,477,837,907 |
| ZAFIRI | | | 414,760,000 | 1,033,429,000 | 16,211,350,333 | | | 17,659,539,333 |
| ZAFICO | | | | 684,940,000 | | | | 684,940,000 |
| ZASCO | 720,155,760 | | | | | | | 720,155,760 |
| S0202: Uhifadhi wa Rasilimali za Baharini | 140,467,350 | 230,000,000 | | | | | | 370,467,350 |
| Uhifadhi Retantion | | 2,699,865,650 | | | | | | 2,699,865,650 |
| **P03: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Uchumi wa Buluu** | **2,243,140,990** | **1,126,894,010** | | | | | | **3,370,035,000** |
| S0301: Utawala na Uendeshaji | 1,161,119,266 | 600,799,734 | | | | | | 1,761,919,000 |
| S0302: Mipango Sera na Utafiti | 193,769,100 | 300,093,900 | | | | | | 493,863,000 |
| S0303: Uratibu wa kazi za Wizara Pemba | 888,252,624 | 226,000,376 | | | | | | 1,114,253,000 |
| **Jumla Kuu** | **4,802,690,000** | **5,611,760,000** | **1,745,140,000** | **3,605,199,000** | **130,255,390,000** | **4,076,365,225** | **58,910,954,775** | **209,007,499,000** |

## Kiambatanisho Nam. 5: Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

| FUNGU | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO YA MAPATO 2026/2027 |
|---|---|---|---|
| 013 - PEMBA | 11610101 | LESENI ZA BIASHARA (LESENI YA VYOMBO VYA UVUVI) | 56,060,000 |
| | 114512102 | MAPATO YA USAFIRISHAJI WA BIDHAA NJE (LESENI ZA UVUVI NA USAFIRISHAJI NJE) | 146,956,000 |
| | 14220258 | ADA ZA VIBALI (LESENI ZA UVUVI NA USAFIRISHAJI NJE) | 127,453,000 |
| | 14220141 | ADA ZA USAJILI (ADA ZA HUDUMA ZA BAHARINI) | 9,000,000 |
| | 14220171 | ADA YA UINGIAJI WA WAGENI (ADA ZA KIINGILIO) | 318,024,000 |
| | | **JUMLA NDOGO** | **657,493,000** |
| 013 - UNGUJA | 11610101 | LESENI ZA BIASHARA (LESENI YA VYOMBO VYA UVUVI) | 185,714,000 |
| | 14512102 | MAPATO YA USAFIRISHAJI WA BIDHAA NJE (LESENI ZA UVUVI NA USAFIRISHAJI NJE) | 275,000,000 |
| | 14220141 | ADA ZA USAJILI (ADA ZA HUDUMA ZA BAHARINI) | 2,276,000 |
| | 14220258 | ADA ZA VIBALI (LESENI ZA UVUVI NA USAFIRISHAJI NJE) | 3,198,000 |
| | 14210147 | LESENI ZA UVUVI NA USAFIRISHAJI NJE (DEEP SEA) | 3,788,772,000 |
| | 14220171 | ADA ZA KIINGILIO CHA WAGENI | 8,293,364,000 |
| | 14310101 | FAINI | 1,290,000 |
| | 14220170 | ADA ZA UTAFITI | 2,463,000 |
| | 14220169 | ADA ZA UTALII WA MICHEZO | 39,233,000 |
| | 14220122 | MAPATO YA NYARAKA ZA ZABUNI | 2,500,000 |
| | | **JUMLA NDOGO** | **12,593,810,000** |
| | | **JUMLA KUU** | **13,251,303,000** |


## Kiambatanisho Nam. 6: Mchanganuo wa Mafunzo ya Muda Mrefu kwa Mwaka 2025/2026

| NAM. | NGAZI YA MASOMO | FANI ANAYOSOMEA | MAHALI | IDADI YA WAFANYAKAZI | MWAKA WA KUMALIZIA MASOMO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Shahada ya Uzamivu (PHD) | Uzamivu wa Sayansi | CANADA | 1 | 2025 |
| 2. | Shahada ya Uzamivu (PHD) | Masuala Ya Bahari (Marine Affairs) | CHINA | 1 | 2028 |
| 3. | Shahada ya Uzamivu (PHD) | Climate Change | KOREA | 1 | 2026 |
| 4. | Shahada ya Uzamili | Public Administration | ZANZIBAR | 1 | 2025 |
| 5. | Shahada ya Uzamili | Fisheries Science | DAR-ES-SALAAM | 1 | 2025 |
| 6. | Shahada ya Uzamili | Master Of Science In Aquaculture | BELGIUM | 2 | 2026 |
| 7. | Shahada ya Uzamili | Master Of International Economic Development | CHINA | 1 | 2027 |
| 8. | Shahada ya Uzamili | Sustainable Fisheries | DAR ES SALAAM | 1 | 2027 |
| 9. | Shahada ya Uzamili | Master Of Sciece In Environmental Studies | ZANZIBAR | 1 | 2026 |
| 10. | Shahada ya Uzamili | Fisheries | CHINA | 1 | 2027 |
| 11. | Shahada ya Uzamili | Master Of Economics And Finance | ZANZIBAR | 1 | 2026 |
| 12. | Shahada ya Kwanza | Accounting And Finance | UGANDA | 1 | 2027 |
| 13. | Shahada ya Uzamili | Accounting And Finance | ZANZIBAR | 1 | 2026 |
| 14. | Astashahada | Project Planning And Managenet | ZANZIBAR | 1 | 2025 |
| 15. | Shahada ya Kwanza | Uchumi Na Maendeleo | ZANZIBAR | 2 | 2028 |
| 16. | Shahada ya Uzamili | Professional Master Program In Fisheries | DAR ES SALAAM | 1 | 2028 |

## Kiambatanisho Nam. 7: Mchanganuo wa Mafunzo ya Muda Mfupi kwa Mwaka 2025/2026

| NAM | AINA YA KOZI | IDADI | MAHALA | TAASISI ILIYOTOA MAFUNZO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | "Value Chain Development for Sustainable Use of Fisheries Resources | 1 | JAPAN | JICA |
| 2. | Warsha ya mafunzo ya tathmini ya mchango wa uvuvi na ufugaji wa viumbe majini | 1 | MALAWI | FAO- NEPAD AGENCY. |
| 3. | Sophos XGS Certified administration | 1 | DAR ES SALAAM | UPI |
| 4. | Mafunzo ya udereva | 1 | DAR ES SALAAM | National institute of transport |
| 5. | Kilimo na ujasiliamali | 1 | CHINA | |
| 6. | Secretarial skills in office management and administration | 1 | MOROGORO | Serengeti east Africa management consultant |
| 7. | Precision Agriculture for Mediterranean Region | 1 | ITALY | Wizara mambo ya nje ya Italy |
| 8. | Mafunzo ya Asset and Inventory management kwa wahasibu, wakaguzi na watunza ghala | 2 | MOROGORO | RFF Zanzibar Inter consultant Ltd |
| 9. | Mafunzo ya usimamizi wa mali za umma | 19 | WIZARANI | Ofisi ya msajili wa hazina |
| 10. | Induction Courses | 11 | IPA | IPA |
| 11. | Mafunzo kuhusu utekelezaji wa programu mtambuka zinazohusiana na Usalama na Afya Mahali pa Kazi. | 235 | WIZARANI | Kamisheni ya Kazi |

**Kiambatanisho Nam. 8: Uzalishaji wa samaki kwa kipindi cha miaka mitano 2020 -2025**



**Kiambatanisho Nam. 9: Uzalishaji wa Mwani kwa kipindi cha miaka mitano 2020 -2025**

